**RIPOTI YA YA CHARITY MKOANI KILIMANJARO TAREHE: 06 APRILI 2026**

**Kituo Kilichotembelewa:** Kituo cha Kulea Watoto Yatima cha ROLINA
**Mahali:** Kwa Sadala – Mkoani Kilimanjaro

## UTANGULIZI

Uongozi wa EX-CASFETA kwa Kushirikiana na Wana wanachama Wote (Group Members) Tuliandaa Tukio la matendo ya huruma lililoitwa Mtoko wa Pasaka kwa Kuchagua kwenda kutembelea Watu wenye uhitaji malaamu ambapo Katika mchakato huo, Kituo cha kulea watoto yatima kiitwacho **ROLINA** Kilichopo Kwa Sadala mkoani Kilimanjaro kilipendekezwa.

Lengo kuu la Charity hii lilikuwa Kuadhimisha miaka 10 ya EX-CASFETA Ushirika , ambapo Uongozi pamoja na wajumbe wakapendekeza kuwa Tukio hili liambatane na Sadaka Ya Upendo na hiari, kila mtu atoe kiasi chochote cha Fedha atakachowiwa ili kwenda kuyagusa maisha ya watoto kwa kuwawezesha Upatikanaji wa mahitaji ya kila siku kituoni.

Mtoko wa Pasaka ilikuwa ni sehemu ya Kumshukuru Mungu kwa Kutuwezesha kutimiza miaka 10 ya Kuwepo Pamoja Kama EX-CASFETA Ushirika lakini Pia malengo mengine ya Mtoko wa Pasaka ilikuwa ni kuendeleza na kudumisha Umoja, mshikamano Miongoni mwa wana EX-CASFETA ikizingatiwa kuwa hakujawahi kutokea tukio lolote lililoandaliwa na EX-CASFETA Ushirika na kutukutanisha na kutuleta wote pamoja kwa Miaka

## 1. HISTORIA FUPI YA KITUO CHA ROLINA

Kituo cha ROLINA kilianzishwa mwaka 1999 na Ndugu Rosemine, kikiwa na dhamira ya kuwalea na kuwahudumia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, Watoto yatima na watoto waliotelekezwa

Jina “ROLINA” limetokana na muunganiko wa majina mawili, yaani *Rosemine* na *Lina*.

Kwa sasa, kituo kinahudumia takribani watoto 30 wa rika mbalimbali, wakiwemo wenye mahitaji maalum. Watoto hawa wanatoka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, Tanzania.

Kituo kinatoa huduma mbalimbali kwa watoto wote wanaoishi na kulelewa kituoni hapo kama vile Chakula, malazi, mavazi, huduma za afya pamoja na elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu(kulipa ada za watoto)

## 2. FEDHA ILIYOKUSANYWA

kwa neema ya Mungu na kujitoa kuchangia kwa Kila Mmoja wetu jumla ya Fedha Taslimu **TSh 1,343,550/=** ilipatikana Kwenye zoezi la kuchangia lililodumu ndani ya mwezi mmoja .

## 3. MATUMIZI YA FEDHA

Katika utekelezaji wa Mtoko wa Pasaka , jumla ya TSh 1,323,000/= zilitumika kwenye matumizi mbalimbali kama ilivyofafanuliwa hapo hapo :-

- Ununuzi wa vyakula (mchele, unga, mafuta n.k.)
- Vifaa vya usafi (sabuni)
- Magodoro
- Gharama za usafiri wa kwenda na kurudi Kituoni
- Chakula cha pamoja kwa washiriki wa Mtoko wa Pasaka

Matumizi haya yalifanyika kwa kuzingatia uhalisia wa mahitaji ya kituo pamoja na Kiasi cha fedha kilichokuwepo.

1.Mchele kg 50@75,000=150,000/=

2.Unga wa ngano kg 25=41,000/=

3.Mafuta ya kula Lt 20=94,000/=

4.Sukari kg 20=65,000/=

5.Peds box 1=36,000/=

6.Stationeries =73,000/=

7.Unga wa ugali kg 20=29,000/=

8.Maharage kg 20@2000=40,000/=

9.Godoro 3@27,000=81,000 (tulipeleka 5 zingine 2 Mhazini wetu alitoa Sadaka)

10.Sabuni ya unga kg 20=26,000/=

11.Juice Caton 2@12000=24,000/=

12.Usafiri 150,000/=

13.Chakula 354,000/=

14.Media 160,000/=

## 4. SALIO BAKI

Baada ya matumizi yote kukamilika, kiasi kilichobaki ni:

**TSh 20,550/=**

## 5. MAHUDHURIO

Katika Mtoko wa Pasaka , wanakikundi EX-CASFETA (CLPD) kutoka Tanzania bara na visiwani walishiriki , Baadhi ya mikoa walikota wanakundi ni kama vile Kilimanjaro, Arusha ,Tanga, Mwanza, Njombe, Mtwara Dar es salaam na Zanzibar.

Ifuatayo ni Orodha ya mahudhurio ya Mtoko wa Pasaka.

1. Nuru Mwakanyamale
2. Yohana Zaya
3. Meshack Malau
4. Chacha Fredy

5. Abednego Sumbe
6. Apha Msaki
7. Agnes Kidugwe
8. Caroline Mremi
9. Lucy Msaki
10. Tumaini Isaya
11. Nancy
12. Juhudi Aloyce
13. Daudi Bigiye
14. Tasimbora Kitomari
15. Riziki Joshua
16. Ellytumaini Rajabu (Dadymedia)
17. Onesmo Mbukwa
18. Evaness Mushi

Aidha, wana CASFETA waliopo chuoni walioshiriki ni:

1. Wilbert Severin Kapinga
2. David Aram
3. Debora Jeremia
4. Juliana Mussa
5. Kelvin aloyce

Vilevile Mchungaji Mlezi wa CASFETA TAYOMI Chuo kikuu cha Ushirika moshi, Mch.Habib Christian Kuya, alialikwa na kuhudhuria kwenye hafla ya Chakula cha Mtoko wa Pasaka.

## 6. MAONI NA MAPENDEKEZO YA WAJUMBE

Katika tathmini ya pamoja baada ya Kutoka kwenye Kituo cha ROLINA , Wajumbe Walikutana katika Viwanja vya KILIHOME kwa ajili ya mazungumzo Mafupi pamoja na Chakula cha Pamoja.

Wajumbe walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo ili kuboresha na kuimarisha umoja wetu:

1. Kuanzishwa kwa miradi ya kudumu ya kiuchumi ili kuongeza vyanzo vya mapato.

2.Kuwekwa kwa mfumo wa uchangiaji endelevu (mfano M-KOBA), utengenezwe Utaratibu wa kumfanya kila mmoja wetu Achangie michango kwa Kutoa kidogo kidogo mfano M-KOBA Ambapo Kila mtu Atakuwa anachangia Kiasi chochote cha fedha anachoweza,kabla ya michango haijaanza kwenye kundi na Ikitokea kuna Changizo kwenye Group hicho kiasi Kinaweza Kutolewa kama mchango wa mhusika.

3.Tutengeneze Action Group kulingana na Kanda Tulizonazo, ili kurahisha Utendaji kazi kwenye Group.

4.Kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwafikia wanachama wasiokuwa Online (mtandaoni)

5.Kufufua wazo kununua Coaster ya CLPD ili kiwe Chanzo kimojawapo cha mapato lakini Pia Itusaidie Kwenye Shughuli zetu pamoja na wenzetu waliopo Chuoni.

6.Tutengeneze Programu maalumu & utaratibu wa kusaidiana Kiuchumi, Kazi na internship kati Yetu

7.Kuimarisha na kudumisha mahusiano mazuri kati ya EX-CASFETA na wana CASFETA waliopo Chuoni , Viongozi wa EX-CASFETA na viongozi waliopo Chuoni Mfano Kuwatembelea, Kuwatia Moyo Nk hii Itasaidia Kutengeneza Mwitikio mzuri Pindi Waliopo Chuo wanapomaliza Na Kuja CLPD(EX-CASFETA)

8.Utaratibu wa kuunda & Kutengeneza Kanda ukishsakamilika kuwepo na Utaratibu wa Watu waliopo kwenye kanda husika kukutana mara kwa mara na Kufanya vikao Pamoja na Ratiba Nyingne watakazokubaliana

9.Kuanzishwa kwa ada ya uanachama ya kila mwezi, ili Kuongeza Vyanzo vya mapato vya CLPD (EX-CASFETA)

10.Tutengeneze Utaratibu wa Kujitangaza ili Tujulikane EX-CASFETA (CLPD ) ni Akina Nani na Tupo kwa ajili ya Malengo gani? Mfano Tuwe na T-shirt Zenu Nk

11.Utengenezwe Utaratibu wa kutambua mchango wa Viongozi na Watu mbalimbali walioutoa, Kuonyesha au Kushiriki kwa Ajili ya CLPD(EX-CASFETA)Kutambua na kuthamini michango ya wanachama na viongozi.

12.Tuweke Utaratibu wa Kwenda CASFETA -CHUONI na Kuongea Nao kuhusu CLPD(EX-CASFETA) ni Nini na Malengo Yetu Makubwa Ni Yapi, Maana Walio Chuo wengi wao hawaelewi kuhusu CLPD Hii itasaidia kutengeneza Mwitikio Mzuri Pindi Wanapomaliza Chuo.

13.Kuanzishwa kwa SACCOS ya umoja.

14.Kuhamasisha Watu/ Tuhamasishane (EX-CASFETA) kushiriki Nahukuhudhuria Matukio mbalimbali Yanayotuhusu

15.Kuendelea kuwaombea, kuwashauri na kuwatia moyo wanaCASFETA waliopo chuoni.

## HITIMISHO

Mungu awabariki Nyote Mliofanikisha mtoko wa Pasaka, kupitia maombi, michango na utayari wa kusafiri na kuhudhuria kwenye Tukio hili

Aidha Tunamshukuru Mungu kupitia Tukio Waandishi wa habari wa Channel ten pamoja na Pazia Tv , Dady media na Seenbaba media Walikuwepo Kwa ajili Ya Kuchukua Matukio.